



Pata uthibitisho wa chanjo yako ya COVID-19

Immunisation history statement yako inarekodi hali yako ya chanjo ya COVID-19

Njia ya rahisi sana kupata taarifa yako ni mtandaoni kwa kutumia yoyote:

- Akaunti yako ya Medicare online kupitia myGov
- Programu ya mkononi ya Express Plus Medicare.

Jinsi ya kupata immunisation history statement yako

Kutumia akaunti yako ya Medicare online kupitia myGov:

1. Ingia kwa myGov na chagua **Medicare**.
2. Kwa sanduku ya **Immunisation history**, chagua **View statement**.
3. Chagua jina lako, na ndipo chagua **View history statement (PDF)**.

Kutumia programu ya mkononi ya Express Plus Medicare:

1. Ingia kwenye programu.
2. Chagua **Immunisation history** kutoka **Services**.
3. Chagua jina lako, na ndipo chagua **View history statement (PDF)**.

Ikiwa huwezi kupata immunisation history statement yako kwenye mtandaoni au unahitaji msaada, pigia simu kwa **1800 653 809**.

Ikiwa huna akaunti ya Medicare mtandaoni

Utahitaji kuunganisha Medicare kwa akaunti yako ya myGov ili kuanzisha akaunti yako Medicare ya mtandaoni.

Ingia kwa, au anzisha, akaunti yako ya myGov kwenye **my.gov.au**

Unaweza basi kuunganisha Medicare kwa kutumia yoyote:

- nambari ya kadi yako Medicare na habari kutoka historia yako ya Medicare
- nambari ya kuunganisha iliyotolewa na Medicare.

Kupata msaada wa kuunganisha Medicare kwa myGov, enda kwa **servicesaustralia.gov.au/medicareguides**

Sasisho habari yako ya mawasiliano ya Medicare

Ni muhimu kuwa habari yako ya mawasiliano ya Medicare imesasishwa. Unaweza kuangalia na kusasisha habari yako kwa kutumia akaunti yako ya Medicare ya mtandaoni au programu ya mkononi ya Express Plus Medicare.

Ikiwa hustahili kwa Medicare au Department of Veterans' Affairs (DVA)

Unaweza kuomba kwa Individual Healthcare Identifier (IHI) kwetu kupata muhtasari wa chanjo kupitia My Health Record. Enda kwa servicesaustralia.gov.au/ihi kwa maelezo zaidi.

Kwa sasisho na ushauri wa COVID-19 wa hivi karibuni, enda kwa australia.gov.au

Kwa habari zaidi

- piga simu kwa Translating and Interpreting Service (TIS National) kwenye **131 450** kuongea nasi katika lugha yako juu ya huduma za Medicare
- enda kwa servicesaustralia.gov.au/ihs kwa habari zaidi katika Kiingereza
- enda kwa servicesaustralia.gov.au/yourlanguage unapoweza kusoma, kusikiliza au kuangalia video na habari katika lugha yako
- tembelea kituo cha huduma.

Kumbuka: simu kutoka simu yako ya nyumbani kwenda nambari za '13' kutoka popote nchini Australia zinatozwa kwa kiwango kamili. Kiwango hicho kinaweza kutofautiana kutoka bei ya simu ya mtaa na kinaweza pia kutofautiana na watoaji huduma ya simu. Simu za nambari za '1800' kutoka simu yako ya nyumbani hazina malipo. Simu kutoka simu za umma na za mkononi zinaweza kupimwa kwa muda wao na kutozwa kwa kiwango cha juu zaidi.